

2. مَدُّ الْجَائِزِ الْمُنْفَصِلِ (Maddul-Jaaiz Al-Munfaswil)

Ni kuwepo herufi ya madd mwisho wa neno, na kufuatiwa na hamzah katika mwanzo wa neno linaloifuatia. Inaitwa **Jaaiz** kwa kuwa huvutwa pia kwa harakah mbili kwa twariyq (njia) nyingine ya Hafsw 'An 'Aaswim *twariyq Twayyibatin-Nashr*. Lakini kwa *twariyq* tunayofundishia ya Hafsw 'An 'Aaswim ambayo ni *twariyq Ash-Shatwabiyyah*, haipasi kuivuta haraka mbili¹ bali hukmu yake ni kuivuta nne au tano. Hivyo ni kwa sababu kuna hukmu nyenginezo zinazohusiana na riwaayah ya Hafsw 'An Aaswim *twariyq Twayyibatin Nashr*, ambazo msomaji anapaswa azifuate zote pindi anapokuwa anafuata twariyq hiyo.

Inaitwa 'Mun-faswil' (inayotengana) kwa vile hamzah inatokea baina ya maneno mawili hivyo inatengana na herufi ya madd.

| Mifano ya maddul-Munfaswil | |
|----------------------------|-----------------------|
| إِذَا أَلْقُوا | تُوبُوا إِلَى اللَّهِ |
| مَا أَمَرَهُمْ | وَمَا أَدْرَاكَ |
| فِيهَا أَبَدًا | وَالَّذِي أَخْرَجَ |

¹Baadhi ya wasomaji hudhania kuwa katika neno هَتَوْلَاءُ kuna madd mbili za 'Waajib Muttaswil'; ukweli ni kuwa asili ya hili neno ni هَا + أُولَاءُ hivyo basi madd ya kwanza ni 'Madd Munfaswil' na Madd ya pili ni 'Madd Muttaswil' lakini zimeandikwa katika neno moja lililoshikamana (muttaswil) na haijuzu kuitenganisha هَا na kuanza kwa neno أُولَاءُ

Tanbihi kuhusu madd hizo mbili; مَدُّ الْمُتَّصِلِ (maddul-muttaswil) na مَدُّ الْمُفْصَلِ (maddul-munfaswil):

Msomaji akiamuwa kurefusha مَدُّ الْمُتَّصِلِ (maddul-muttaswil) kwa haraka nne katika qiraa-ah chake, inapasa pia avute مَدُّ الْمُفْصَلِ (maddul-munfaswil) kwa haraka nne. Na akiamu kuivuta مَدُّ الْمُتَّصِلِ (maddul-muttaswil) kwa harakah tano, basi inampasa avute harakah tano katika مَدُّ الْمُفْصَلِ (maddul-munfaswil). Inapasa afanye hivyo katika usomaji wake wote.